

## **TAARIFA YA IDARA YA ARDHI NA MALIASILI KWA KIPINDI CHA KUANZIA OKTOBA HADI DESEMBA 2016/2017**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Idara ya Ardhi na Maliasili kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Disemba, 2016. Taarifa ilieleza kuwa Idara ya Ardhi na Maliasili ina jumuisha sehemu 5 ambazo ni: Ardhi Utawala, Upimaji na Ramani, Mipango Miji, Misitu na Wanyamapori. Katika kipindi Oktoba – Disemba, 2016, Idara ilijishughulisha na kazi mbalimbali kama zilivyooneshwa kwenye taarifa za kila Sehemu.

### **2.0. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SEHEMU**

#### **2.1 SEHEMU YA ARDHI UTAWALA, UPIMAJI NA RAMANI, MIPANGO MIJI NA UTHAMINI**

Taarifa ilieleza kuwa kwa kipindi cha Oktoba – Disemba 2016, Sekta ya Ardhi imetekeliza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

##### **2.1.1 UKUSANYAJI WA KODI YA ARDHI**

*Makusanyo ya kodi ya Ardhi Octoba – Decemba, 2016*

<b>Na</b>	<b>MWEZI</b>	<b>KIASI (Tshs)</b>
1	Octoba	6,871,114.00
2	Novemba	3,726,920.00
3	Desemba	15,081,270.00
	<b>Jumla</b>	<b>25,679,304.00</b>

##### **2.1.2 MAKUSANYO YA MAPATO YA GHARAMA ZA UPIMAJI VIWANJA**

Taarifa ilieleza kuwa kati ya wananchi walioneshwa viwanja, baadhi yao wamefika ofisi ya Ardhi na kupewa gharama halisi za kiwanja husika na baadae kwenda Benki kulipia sehemu ya garama ya viwanja husika. Kwa kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2016* Jumla ya Tshs. **89,228,624/=** zimekusanywa kama mapato ya Halmashauri kutokana na gharama za upimaji na fidia katika eneo la Nangando na Likongowele. Mapato hayo tayari yameshaingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri.

*Makusanyo yatokanayo Na malipo ya viwanja Kwa kipindi cha Octoba – Decemba, 2016*

<b>Na</b>	<b>MWEZI</b>	<b>KIASI (Tshs)</b>
1	Octoba	6,593,094.00
2	Novemba	7,845,750.00
3	Desemba	74,789,780.00
	<b>Jumla</b>	<b>89,228,624.00</b>

### **2.1.3 KUFANYA TATHIMINI YA MALI ZA WANANCHI KATIKA ENEO LA NANGANDO**

Taarifa ilieleza kuwa zoezi la Ukaruzi mashamba ya mikorosho ya wananchi kwa ajili ya fidia katika eneo la Mitambo ya kuzalisha umeme wa TANESCO liwale limefanyika. Jumla ya mashamba 12 ya wananchi yamefanyiwa uthamini wa fidia. Aidha Taarifa ya uthamini ya Mali za wananchi tayali imeandaliwa na inasubiri kupelekwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa serikali.

### **2.1.4 KUFANYA MKUTANO NA WANANCHI KATIKA KIJIJI CHA MUNGURUMO**

Taarifa ilieleza kuwa Mkurugenzi na timu ya Wataalamu walifika katika maneo ya Mungurumo na kufanya mikutano ya uhamasishaji katika maeneo ambayo upimaji unatarajiwu kufanyika. Katika mkutano huo viongozi wa vitongoji waliagizwa kuwatambua wakazi waliopo kwenye maeneo ambayo tunatarajia kupima viwanja na kubainisha kati ya wale waliouziwa vipande vya ardhi na wamailiki wa mashamba. Baada kutambuliwa Ofisi ya ardhi inatarajia kuanza kufanya uhakiki wa wakazi hao ili zoezi la upimaji lifanyike.

### **2.1.5 KUFANYA UHAKIKI WA WAFANYABIASHARA AMBAO WANAFANYA BIASHARA KATIKA ENEO LINALOZUNGUKA UWANJA WA MPIRA (“ENEO LA ZEIN”)**

Taarifa ilieleza kuwa Tarehe 15.12.2016 zoezi la uhakiki wa wafanyabiashara wote ambao wanafanya biashara katika eneo Uwanja Wa Mpira (“Eneo La Zein”) lilifanyika. Lengo la uhakiki huo ni kiwatambua wafanyabiashara hao ili waweze kupewa kipaumbele katika ugawaji viwanja mara baada ya zoezi la upimaji litakapokamilika jumla ya wafanyabiashara wapatao 148 walihakikiwa.

### **2.1.6 KUTAYARISHA HATI MILIKI ZA VIWANJA ZA MUDA MREFU.**

Taarifa ilieleza kuwa Rasimu za Hati miliki za viwanja za muda mrefu 45 zimeandaliwa, hati hizo zitapelekwa kwa Kamishina wa Ardhi msaidizi wa Kanda ya Kusini kwa ajiliya kuidhinishwa na kusajiliwa na Msajili wa Nyaraka.

### **2.1.7 KUTATUA MIGOGORO YA ARDHI**

#### **2.1.7.1 MGOGORO WA MPAKA KATI YA KIJIJI CHA TURUKI NA LIKOMBORA.**

Taarifa ilieleza kuwa tulipokea barua kumb Na.LIK/H/K/01 ya tarehe 15.09.2016 ya kuwepo kwa mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Turuki na Likombora, na chanzo cha mgogoro huo ilikuwa ni eneo ambalo lilijengwa mnara wa simu wa mtandao wa Airtel. Kampuni ya Airtel walifika katika kijiji cha Turuki na kubaini eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mnara husika, na baadae wahusika wakaingia mkataba na Kijiji cha Turuki kama wamiliki wa eneo hilo. Hata hivyo upande wa Kijiji cha Likombora wakaanza kudai kuwa mnara huo upo upande wa Kijiji chao na siyo kijiji cha Turuki, ndipo wakaomba msaada wa wataalamu toka Wilayani kwa lengo la kupata ufumbuzi wa suala hili.

Tarehe 4.10.2016, Timu ya wataalam kutoka wilayani ilifika katika kijiji cha Turuki kwa lengo la kupata suluhu ya mgogoro huo, Halmashauri za vijiji husika zilikutanishwa na kujadili juu ya Mgogoro uliopo. Aidha wataalamu waliwafahamisha

njia ambayo ingetumika katika kubaini ni upande gani wa kijiji ambao mnara huo umejengwa. Kutachukuliwa (Jira) Coordinate katika eneo palipojengwa Mnara na baadae zitaiingizwa kwenye ramani za vijiji husika ambayo ipo katika computa na jibu litapatikana.

Baada ya kikao hicho Wataalamu pamoja na wawakilishi wa pande zote mbili walifika katika eneo palipojengwa mnara na kuchukua jira (coordinates) kwa kuzunguka pande zote nne za mnara huo, na ziliingizwa katika ramani ya vijiji hivyo na kuonesha kuwa mnara huo umejengwa katika kijiji cha Likombola na sio kama ilivyodhaniwa hapo awali. Mwisho pande zote mbili zilielekezwa na kuelewa.

### **2.1.7.2 UTATUZI WA MGOGORO KATI YA KIJIJI CHA NAMBINDA NA MLEMBWE**

Taarifa ilieleza kuwa tarehe 27.10.2016 Mh Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi pamoja na Wataalamu walifanya ziara katika kijiji cha Mlembwe na Nambinda. Pande mbili zilikutanishwa na kujadili juu ya Mgogoro huo. Chanzo cha mgogoro huo ni madai kwa upande wa Mlembwe kwamba hakukua na makubalino ya mpaka kati ya vijiji hivyo, kwa upande wa kijiji cha Nambinda wao wanasema kulikuwa na makubalino ambayo yalibainisha mipaka kati ya pande zote mbili. Hata hivyo kwa mujibu wa muhtsari wa kikao cha tarehe 05.11.2008 mipaka ya vijiji husika ilijadiliwa na kuainisha. Hivyo wajumbe walielekezwa kuridhia muafaka huo wa tarehe 05.11.2008. Sababu zinazopelekea migogoro hii kutokea ni pamoja faida zinazotokana na uwekezaji katika rasilimali zilizopo kwenye vijiji husika, kijiji kimoja kinapokosa manufaa ndipo kinaanzisha mgogoro. Sababu nyingine zimetokana na kutopima kwa wakati vijiji ambavyo vimegawanyika mara baada ya Kitongoji ndani ya kijiji kukua na kuwa kijiji.

### **2.1.7.3 UTATUZI WA MGOGORO KATI YA KIJIJI CHA KIPELELE NA NGUMBU**

Taarifa ilieleza kuwa Tarehe 30.6.2016, Timu ya Wataalam ilikutana Kibutuka na pande mbili zenye Mgogoro kwa lengo la kupata suluhu ya mgogoro wa Mpaka kati ya Kijiji cha Kipelele na Ngumbu. Pande mbili zilikutanishwa na kujadili juu ya Mgogoro huo. Chanzo cha mgogoro huo ni madai kwa upande wa Kipelele kwamba hawautambui mpaka kati yake na Kijiji Ngumbu. Hata hivyo siku hiyo muafaka haukupatikana, hii ilitokana na madai toka upande wa kijiji cha Kipelele kudai Kijiji cha Mirui nacho kishirikishwe kama shahidi katika utatuzi wa mgogoro huo, pia wanakijiji walidai kwamba hawana imani na ramani itakayotumika katika utatuzi wa mgogoro huo. Hata hivyo ilipangwa siku nyingine kwa ajili ya kupata suluhu ya Mgogoro huo.

## **2.2 SEHEMU YA MISITU**

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi Julai- Septemba, 2016, sehemu ya misitu kwa kushirikiana na Wadau wengine imetekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga uhifadhi wa rasilimali za misitu katika maeneo ya Wilaya kama zifuatavyo:

- I. Kusimamia uvunaji na ukusanyaji wa mapato yanatokanayo na mazao ya misitu kwa upande wa Serikali kuu, Halmashauri na Vijiji.
- II. Kufanya doria kudhibiti uvunaji holela wa mazao ya misitu.

- III. Kupitisha mipango ya usimamizi wa misitu na sheria ndogo kwenye vijiji 8 na Mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji 5.
- IV. Kuhamasisha shughuli za upandaji miti.
- V. Kusaidia vijiji kuchakata mazao ya misitu katika misitu yao kupata faida zaidi.

### **2.2.1. KUSIMAMIA UVUNAJI WA MAZAO YA MISITU NA UKUSANYAJI WA MADUHULI**

#### **2.2.1.1. KUSIMAMIA UVUNAJI WA MAZAO YA MISITU**

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi husika, Wataalamu wa misitu kwa kushirikiana na Halmashauri za vijiji kuitia Wajumbe wa Kamati za Maliasili, walisimamia uvunaji wa mazao ya misitu katika maeneo yao ya vijiji. Jumla ya leseni **32** za kupasua mbao / kuvuna magogo ya miti mchanganyiko zenyne mita za ujazo **808** zikiwa na thamani ya **Tzs. 184,942,140/-** zilitolewa katika maeneo ya vijiji kumi (10).

*Jedwali Na. 3. Orodha ya leseni zilizotolewa kipindi cha Julai hadi Septemba 2016.*

NA .	ENEON LA UVUNAJI	IDADI YA LESENI	UJAZO WA LESENI( M <sup>3</sup> )	AINA YA MITI ILIYOVUNWA	THAMANI YA LESENI (TZS)
1.	Mirui	6	170.00	Mninga/Mkongo	40,038,400.00
2.	Barikiwa	3	65.00	Mninga/Mkongo	15,308,800.00
	Barikiwa	1	30.00	Msekeseka/Paurosa	7,065,600.00
3.	Kikulyungu	3	69.00	Mninga/Mkongo	16,250,880.00
	Kikulyungu	1	30.00	Msekeseka/Paurosa	7,065,600.00
4.	Mkutano	4	100.00	Mninga/Mkongo	23,552,000.00
5.	Kimambi	4	87.00	Mninga/Mkongo	20,490,240.00
6.	Ndunyungu	1	26.00	Mtondo	4,592,700.00
7.	Ndapata	3	100.00	Mninga/Mkongo	23,552,000.00
8.	Chimbuko	1	30.00	Mtondo	5,299,200.00
	Chimbuko	3	65.00	Mninga/Mkongo	15,308,800.00
9.	Luwele	1	16.00	Mninga/Mkongo	3,768,320.00
10.	Darajani	1	20.00	Msufi pori	2,649,600.00
	<b>JUMLA</b>	<b>32</b>	<b>808</b>		<b>184,942,140.00</b>

Pamoja na leseni zilizotolewa, kulikuwa na hati za madai zilizotolewa kwa ujazo wa ziada wa mbao na magogo wa mita za ujazo 227.97. Hivyo jumla ya mita za ujazo 1,035.97 za miti mchanganyiko zilivunwa katika kipindi hiki.

Aidha katika kipindi hiki, vijiji vilivyokamilisha mchakato wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu vilitoa leseni za uvunaji wa mbao na magogo katika misitu yao ya vijiji. Jumla ya leseni **5** zenyе ujazo wa mita 118 na thamani ya shilling **27,791,360/-** zilitolewa.

NA	ENEO LA UVUNAJI (KIJINI)	IDADI YA LESENI	UJAZO WA LESENI(M <sup>3</sup> )	AINA YA MITI ILIYOVUNWA	THAMANI (TZS)
1.	Nahoro	2	40	Mkongo na Mninga	9,420,800.00
2.	Nangano	1	17	Mkongo na Mninga	4,003,840.00
3.	Kitogoro	1	41	Mkongo na Mninga	9,656,320.00
4	Mtawatawa	1	20	Mkongo na Mninga	4,710,400.00
	<b>JUMLA</b>				<b>27,791,360.00</b>

#### **2.2.1.3. KUKUSANYA WA MAPATO YA SERIKALI KUU NA HALMASHAURI YA WILAYA**

Taarifa ilieleza kuwa Sambamba na utoaji wa leseni na hati za madai za kuvuna miti na magogo, mapato mengine yaliyokusanywa yalitokana na ada za usajili wa biashara ya mazao ya misitu, fomu za maombi ya usajili na leseni, vibali vyta kusafirishia mazao ya misitu, tozo za samani za mazao ya misitu na mkaa.

Jumla ya shillingi Millioni mia mbili sabini na nane mia mbili ishirini na tatu elfu mia sita kumi na tatu na senti ishirini na tano (**278,223,613.25**) zilikusanywa katika kipindi hiki. Kati ya fedha hizo **Tzs. 244,597,794/-** ni makusanyo ya Wakala wa Huduma za misitu Tanzania, **Tzs 15,240,078/-** ni asilimia 5 ya ada ya upandaji miti na **Tzs. 18,385,741.25** ni asilimia 5 ya ushuru wa Halmashauri

*Jedwali Na. 4. Makusanyo ya mapato yatokanayo na mazao ya misitu kipindi cha Julai hadi Septemba, 2016,*

MWEZI	MAPATO YA SERIKALI KUU (TFS – TZS.)	ADA YA UPANDAJI MITI (TaFF-TZS.)	MAPATO YA HALMASHAURI (TZS.)	JUMLA YA MAPATO (TZS.)
OKTOBA	103,577,553.00	7,778,299.00	7,120,524.00	118,476,376.00
NOVEMBA	58,652,330.00	3,578,264.00	5,809,041.25	68,039,635.25
DISEMBA	82,367,911.00	3,883,515.00	5,456,176.00	91,707,602.00
JUMLA	244,597,794.00	15,240,078.00	18,385,741.25	278,223,613.25

#### **2.2.2. KUFANYA DORIA NA UUZAJI WA MAZAO YA MISITU YALIYOTAIFISHWA.**

##### **2.2.2.1 KUFANYA DORIA**

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi hiki, doria zimefanywa na watumishi wa TFS Wilaya katika maeneo ya vijiji vya Mtawatawa, Kimambi, Naujombo, Kiangara, Kichonda, Ndunyungu, Nangano na Nyera. Jumla ya mbaao mchanganyiko 490 zimekamatwa na kuhifadhiwa maeneo ya Selous.

Katika kipindi hiki Idara ya Maliasil ilifanya doria katika maeneo mbalimbali ya misitu kama ifuatavyo:

Tarehe 17 - 18.10.2016, doria ilifanyika katika msitu wa kijiji cha Mtawatawa ambapo jumla ya mbaao 736 mchanganyiko za Mkongo, Mninga na Msufi pori zilikamatwa. Kati ya mbaao hizo, vipande 292 zilikamatwa na Watumishi wa Idara ya Misitu na zimehifadhiwa Bomani. Mbao zingine 444 zilikamatwa na Wanakijiji wenyewe na kuzihifadhi kijijini.

Mtuhumiwa wa uhalifu huo ni Ndg. Donald Mboya (Mangi) ambaye awali alikuwa ni mteja halali katika uvunaji wa mazao ya misitu katika kijiji hicho. Mbao zote zimetaifishwa na mtuhumiwa ametozwa faini kwa makosa yake na kunyang'anywa vifaa viliviyotumika.

Tarehe 16 na 18.12.2016, doria nyingine ilifanyika katika msitu wa kijiji cha Nanjegeja ikiongozwa na Watumishi wa Idara ya Maliasili. Katika doria hiyo mbaao 14 za msufi, magogo 7 na mti 1 ulioangushwa tayari kwa maandalizi ya kulengetwa vilikamatwa katika eneo la msitu wa Nanjegeja na magogo 4 yalikamatwa eneo la msitu wa kijiji cha Turuki. Uhalifu umefanywa na Zubeda Robert Kigogo aliyepewa kibali na Halmashauri ya kijiji cha Nanjegeja kuvuna mbaao 300 za ujenzi bila kufuata taratibu za Kisheria.

Mtuhumiwa ametaifishiwa mali zote alizotumia katika uvunaji na kutozwa faini pamoja na kurudisha ghamama za doria. Jumla ya shillingi 1,805,000/- zimelipwa Halmashauri ya Wilaya Liwale.

### **2.2.2.2 KUUZA MAZAO YA MISITU YALIYOTAIFISHWA**

Taarifa ilieleza kuwa Mnada haujafanyika kwa mbaao zilizokamatwa na TFS.

Katika kipindi hiki, mauzo ya mbaao zilizokamatwa katika misitu ya vijiji yalifanyika kama ifuatavyo:

- ❖ Kijiji cha Nangano kiliuza mbaao 151 za msufi pori na kupata shillingi **2,733,100/-**
- ❖ Kijiji cha Mtawatawa kiliuza mbaao za Mkongo, Mninga na Msufi na kupata kama mapayo ya kijiji shillingi **6,692,940/-**

### **2.2.3. KUSAIDIA VIJIJI KUCHAKATA MAZAO YA MISITU VYENYEWE KUONGEZA THAMANI**

#### **YA MAZAO YA MISITU.**

Taarifa ilieleza kuwa kupitia Mpango wa Usimamizi wa Misitu wa jamii, LIMAS na MCDI imesaidia kwa majaribio vijiji 2 vya Litou na Mikunya kuchakata mazao ya misitu vyenyewe na kuuza mbaao. Mradi umeviwezesha vijiji kukata leseni ya biashara, usajili na usajili wa eneo la kuuzia (Timber Yard)

Kwa kuanzia kila kijiji kilichakata mita za ujazo **71** za Mninga na Mkongo kwa kutumia mashine za **Ding Don**.

Kijiji cha Litou kiliuza jumla ya mbaao **481** kwa mteja aliyeitwa James Rafael Wapalila kwa thamani ya shillingi **18,070,000/-** na

Kijiji cha Mikunya kiliuza jumla ya mbaao **598** kwa Hassani Tengeneza na kujipatia shillingi **21,241,000/-**

## **2.2.4 KUPITISHA MIPANGO NA SHERIA NDOGO ZA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISTU NA**

### **MATUMIZI BORA YA ARDHI.**

Tarehe 16.11.2016, Baraza la Madiwani lilipitisha Mipango ya Usimamizi wa Misitu na Sheria ndogo za vijiji 8 vya Ngunja, Ngongowele, Mikuyu, Mihumo, Likombora, Turuki, Kiangara na Kibutuka na Mipango na Sheria ndogo za Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 5 vya Ngongowele, Mikuyu, Darajani, Mihumo na Kiangara.

Hatua inayofuata ni kusainiwa kwa Sheria ndogo za Usimamizi wa Misitu na Matumizi Bora ya Ardhi na Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa Halmashauri kwa hatua nyingine.

## **2.2.5 KUHAMASISHA SHUGHULI ZA UPANDAJI MITI**

Katika kipindi hiki shughuli za kuhamasisha kampeni ya upandaji miti zilifanyika. Mionganii mwa shughuli zilizofanyika ni kama ifuatavyo:

- Kuangalia maendeleo ya vikundi ambavyo msimu wa mwaka 2015/16 vilipewa mafunzo ya bustani na kugawiwa vifaa vya kukuzia miche ya miti.
- Kuhamasisha shughuli za ukuzaji wa miche ya miti na upandaji miti katika vikundi vilivyoonesha mwamko wa mafanikio na kuendeleza hamasa kwa baadhi ya shule za sekondari na msingi.
- Ununuzu wa vifaa vya bustani, mbegu na viriba vya kukuzia miche ya miti na kuvisambaza kwenye vikundi na kwenye mashule.
- Kufanya mafunzo ya kutunza na kukuza bustani za miche ya miti kwenye shule za sekondari za R.M.Kawawa, Liwale, Barikiwa, Milina, Anna Magowa, Nikodemas Banduka na Mihumo, shule ya msingi Kambarage na vikundi vya mazingira vya Barikiwa, Naluleo na Liwale (Nangando).

## **2.3. SEHEMU YA WANYAMAPORI**

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi hiki, sehemu ya wanyamaporii ilijishughulisha na kazi zilizolenga kutatua kero za wananchi katika kudhibiti wanyamaporii wakali na hatari kwa Maisha ya binadamu. Leseni za uwindishaji wa kienyeji zimesitishwa kwa miaka miwili.

### **2.3.1. KUDHIBITI WANYAMAPORI WAKALI NA HATARI KWA MAISHA YA**

#### **BINADAMU.**

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2016 hali ya wanyama ni kama inavyooneshwa kwenye majedwali yafuatayo:

#### ***Wanyama waharibifu wa mazao.***

Tarehe	Kijiji	Aina ya mnyama	Uharibifu uliofanyika	Hatua zilizochukuliwa
02.11.2016	Barikiwa	Tembo	Kuliwa mashamba ya korosho Tandamanga	Askari walikwenda na kuwafukuza
08.11.2016	Barikiwa	Tembo	Mashamba ya korosho Tandamanga	Askari walienda na kuwafukuza

*Wanyama wakali kwa maisha ya binadamu*

Tarehe	Kijiji	Aliyeua wa	Aliyejeru hiwa	Jinsi a	Um ri	Kabila	Mnyama aliyehusika	Hatua zilizochukuliwa
01.11.2016	Mirui	Hakuna	Hakuna	-	-	-	Simba	Askari wameenda simba hakuonekana
25.11.2016	Kipelele	Hakuna	Shazil Zuberi Limoge	Me	17	mngindo	Chui	Askari walikwenda na chui ameuawa na wananchi.

*Jedwali Na.7. Hali halisi ya risasi hadi tarehe 31, Disemba, 2016*

Na	AINA YA RISASI	SALIO ANZIA (01.10.2016)	RiSASI ZILIZONUNULIWA (01.10.2016- 31.12.2016)	RISASI ZILIZOTUMIK A (01.10.2016- 31.12.2016)	SALIO. 31.12.2016
1	458 mm	2	0	0	2
2	375 mm	5	0	0	5
3	303 mm	15	0	13	2
4	30.06 mm	65	0	0	65
5	SHOT GUN	102	0	0	102
6	22 HONET	34	0	0	34
7	SAR	0	0	0	0
8	404mm	0	0	0	0
9	Bastola	6	0	0	6
	<b>Jumla</b>	<b>229</b>	<b>0</b>	<b>13</b>	<b>216</b>

**NB:** Bado risasi 25 zipo kituo cha Polisi Kilwa)

*Bunduki na risasi zilizo polisi Kilwa*

Na.	Jina la Askari	Ainaya Bunduki	Idadi ya risasi	Maelezo
1.	Abdallah Namwewe	30.06	15	Zipo Polisi Kilwa
2.	Abdallah Namwewe	303	10	Zipo polisi Kilwa
	<b>Jumla</b>		<b>25</b>	

**2.3.2 TAARIFA YA UWINDAJI JUMUIYA YA MAGINGO**

Taarifa ilieleza kuwa Tarehe 21.10.2016, Jumuiya ya Magingo imempokea Mwindishaji toka Kampuni ya “White Lion”kuwinda kwenye kitalu cha Hokororo kwa kibali Na. 2003759 toka Wizara ya Maliasili na Utalii (Idara ya Wanyamapori) kwa ajili ya kuwinda wanyama saba kama ifuatavyo: Nyati 2, Nyumbu 2, Kongoni 1, Punda milia 1 na Swala 1.

Mtumishi aliyesimamia uwindishaji huo ni Ndg. Zuberi Kinderu toka Halmashauri ya Liwale. Tarehe 15.12.2016, Jumuuya ya Magingo imempokea Mwindishaji aitwae Salimu Mohamed Salimu aliyepelekwa Kitalu cha Hokororo na Kampuni ya ‘White Lion’ kwa leseni Na. 2003826 iliyotolewa na Wizara ya Maliasili. Wanyama walioruhusiwa kuwindwa ni 3, ambaao ni Palaala 1, Pofu 1 na Chui 1. Aliyesimamia uwindaji huo ni Mtumishi Zuberi Kinderu.

### **3.0.CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA**

1. Ukoefu wa watumishi katika sehemu za Wanyamapor, Upimaji na Ramani.
2. Uvamizi wa wanyamapor hususani Tembo, katika maeneo ya mashamba.
3. Ukataji wa misitu kwa kilimo cha ufuta na uchomaji misitu moto.

### **4.0. MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

- Kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya uchomaji moto wa misitu na mapori.
- Kutoa elimu juu ya kilimo kinachozingatia mbinu za kitaalamu.
- Kuendelea kuwasiliana na idara Kuu ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kupata watumishi wapya.

Katika kujadili taarifa hiyo yafuatayo yalijitokeza:-

#### **i.Hati Milki**

Mjumbe mmoja alitoa hoja ya kutaka kujua katika Wilaya ya Liwale kuna watu wangapi wenye Hati Milki

Hoja hiyo ilijibiwa kuwa kwa sasa idadi halisi hakuna ila itafanyiwa kazi na kuwasilishwa kikao kijacho. Hata hivyo ilielezwa kuwa watu wengi hawataki kulipia hati milki na wengine wamejenga kwenye maeneo yasiyo na Ramani.

#### **ii.Uvunaji wa Mazao ya Misitu**

Mjumbe mmoja alitaka kujua utatibu wa kuvuna mazao ya misitu kwani kuna wengine wanavuna miti ambayo haipo kwenye Leseni

Maelezo yalitolewa Ofisi bado haipokea changamoto hiyo na kwamba waombaji wanapoomba kuvuna mazao ya misitu wanapewa leseni kulingana na maombi yao.

## **PENDEKEZO LA KUBADILI MATUMIZI YA KIWANJA CHA MAKABURI**

### **MATUMIZI YA OFISI YA TRA NA MAHAKAMA LIWALE**

Kumekuwepo na mahitaji viwanja kwa ajili ya matumizi ya ofisi katika maeneo ya ya Mjini Liwale. Kwa wakati tofauti tumepokea maombi ya viwanja kwa ajili Matumizi ya Ofisi toka katika taasisi mbalimbali za serikali,viwanja vinavyoitajika ni vile vilivopo katika maeneo ambayo ni rahisi kufikia. Eneo husika lilipangwa kwa matumizi ya makaburi hata hivyo lipo karibu na makazi ya watu na linaweza kutumika kwa matumizi ya ofisi. Lipo eneo lingine ambalo lilipangwa na kupimwa kwa matumizi ya makaburi maeneo ya Nangando,Hivyo kulibadili eneo hili hakutaathili maitaji ya maeneo kwa ajili ya kuzikia.

## **PENDEKEZO**

Baada ya maelezo hayo yaliwasilishwa mapendekezo ya kubadili matumizi ya eneo tajwa toka matumizi ya makabuli kuwa matumizi ya ofisi . Mara baada ya kufanyiwa marekebisho eneo husika litagawanywa kwa matumizi ya ofisi mbalimbali na hivyo kukizi maitaji ya ofisi kwa sasa.

Baada ya mjadala wajumbe walipitisha pendekezo la kubadili matumizi ya Kiwanja cha Makaburi matumizi ya ofisi ya TRA na Mahakama Liwale ili liwasilishwe kwenye Mkutano wa Baraza la Hlmashauri kwa maamuzi

Naomba kuwasilisha